# FUNZO LA 57

1. Kwa nini Yesu alichoka?
-Ijapokuwa Yesu alikuwa Mungu kamili, pia alikuwa mwanadamu kamili.

2. Je, Yesu aliwezaje kuamuru upepo na bahari zitulie?
-Kwa sababu Yesu alikuwa Mungu.

3. Kwa nini upepo na bahari vilipaswa kumtii Yesu?
-Kwa sababu ni Yesu aliyeumba upepo na bahari.

4. Je, yule mtu aliyepagawa na mapepo aliweza kujiokoa mwenyewe kutoka kwa nguvu za mapepo wote waliomdhibiti?
-La.

5. Je, wengine waliweza kumwokoa mtu huyu kutoka kwa nguvu za mapepo yote waliomdhibiti?
-La.

6. Je, tunajuaje kwamba mapepo hutuchukia sisi watu?
-Kwa sababu mapepo yalimlazimisha yule mtu kuishi kwenye mapango ambayo watu walizikwa.
-Kwa sababu mapepo yalimlazimisha yule mtu ajikate.

7. Ni nani mkuu wa mapepo yote?
-Shetani.

8. Ni nani aliye mkuu kuliko Shetani na mapepo yake?
-Yesu ambaye ni Mungu.



9. Wakati nguruwe wote walikufa, kwa nini mapepo hayakufa?
-Kwa sababu mapepo ni roho.
-Kwa sababu mapepo hayana mwili kama watu au wanyama.

10. Ni nani aliyemweka huru huyo mtu kutoka kwenye kifungo cha mapepo?
-Yesu.

-Muda mchache baadaye, Yesu na wanafunzi wake walivuka hadi pwani ya mbali ya Ziwa la Galilaya.

Tusome Yohana 6:1-2

1-Baada ya hayo Yesu alikwenda zake ng'ambo ya Bahari ya Galilaya, nayo ndiyo ya Tiberia.
2-Na mkutano mkuu wakamfuata, kwa sababu waliziona ishara alizowafanyia wagonjwa.

-Kwa nini umati mkubwa ulimfuata Yesu?

-Kwa sababu walitaka kuona ishara zaidi za miujiza ambazo Yesu alikuwa amezifanya kwa wagonjwa.

Tusome Yohana 6:3

3-Naye Yesu akakwea mlimani, akaketi huko pamoja na wanafunzi wake.

-Ijapokuwa Yesu na wanafunzi Wake walipanda juu ya mlima, umati mkubwa ulimfuata.

-Umati ulikuwa mwingi sana hivi kwamba kulikuwa na zaidi ya watu elfu tano.

-Kisha, Yesu alimuuliza mmoja wa wanafunzi wake, Filipo, swali.

Tusome Yohana 6:5-7

5-Basi Yesu alipoinua macho yake akaona mkutano mkuu wanakuja kwake, alimwambia Filipo, Tununue wapi mikate, ili hawa wapate kula?
6-Na hilo alilinena ili kumjaribu; kwa maana alijua mwenyewe atakalotenda.
7-Filipo akamjibu, Mikate ya dinari mia mbili haiwatoshi, kila mmoja apate kidogo tu.

-Kwa nini Yesu alimuuliza Filipo swali hili?

-Yesu alitaka kumjaribu Filipo, kwa maana Yesu alikuwa tayari anajua atakachofanya.

Tusome Yohana 6:8-9

8-Wanafunzi wake mmojawapo, Andrea, nduguye Simoni Petro, akamwambia,
9-Yupo hapa mtoto, yuna mikate mitano ya shayiri na samaki wawili, lakini hivi ni nini kwa watu wengi kama hawa?

-Wanafunzi wa Yesu hawakujua jinsi watakavyowalisha watu wote.



-Hivi ndivyo Yesu aliwaambia:

Tusome Yohana 6:10-13

10-Yesu akasema, Waketisheni watu. Na mahali pale palikuwa na majani tele. Basi watu waume wakaketi, wapata elfu tano jumla yao.
11-Basi Yesu akaitwaa ile mikate, akashukuru, akawagawia walioketi; na kadhalika katika wale samaki kwa kadiri walivyotaka.
12-Nao waliposhiba, aliwaambia wanafunzi wake, Kusanyeni vipande vilivyobaki, kisipotee cho chote.
13-Basi wakavikusanya, wakajaza vikapu kumi na viwili, vipande vya mikate mitano ya shayiri vilivyowabakia wale waliokula.

-Baada ya Yesu kumshukuru Mungu Baba, Akaimega ile mikate na samaki, akawapa wanafunzi wake wape watu.

-Yesu alipoanza kuwalisha watu, alikuwa na mikate mingapi na alikuwa na samaki wangapi?

-Mikate mitano na samaki wawili.

-Yesu alilisha watu wangapi na mikate mitano na samaki wawili?

-Zaidi ya watu elfu tano.

-Je, Yesu aliwezaje kulisha watu zaidi ya elfu tano na mikate

mitano na samaki wawili?

-Kwa sababu Yesu ni Mungu.
-Kwa sababu Yesu anaweza kufanya chochote.

-Baada ya watu wote kula, walisema nini?

Tusome Yohana 6:14-15

14-Basi watu wale, walipoiona ishara aliyoifanya, walisema, Hakika huyu ni nabii yule ajaye ulimwenguni.
15-Kisha Yesu, hali akitambua ya kuwa walitaka kuja kumshika ili wamfanye mfalme, akajitenga, akaenda tena mlimani yeye peke yake.

-Kwa nini watu walitaka kumfanya Yesu mfalme?

-Kwa sababu walitaka Yesu awape chakula kila wakati.

-Je, watu walitaka Yesu awaokoe kutoka kwa dhambi, kifo, na Shetani?
-La.

-Walikuwa wakifikiria tu matumbo yao.

-Kwa nini Yesu hakutaka kuwa mfalme wa watu hao?

-Kwa sababu Yesu alijua kwamba mioyo ya watu hao ilikuwa mibaya.



-Kwa sababu Yesu alijua kwamba watu hao walitaka tu Yeye awape chakula.

-Kwa sababu ya watu, Yesu alienda peke yake.

-Jioni ilipofika, wanafunzi wa Yesu waliingia kwenye mashua, na kuanza kuvuka ziwa la Galilaya.

Tusome Yohana 6:16-21

16-Hata ilipokuwa jioni wanafunzi wake wakatelemka baharini
17-wakapanda chomboni, wakaanza kuivuka bahari kwenda Kapernaumu. Nako kumekwisha kuwa giza, wala Yesu hajawafikia.
18-Na bahari ikaanza kuchafuka kwa kuvuma upepo mkuu.
19-Basi wakavuta makasia kadiri ya maili tatu nne, wakamwona Yesu anakwenda juu ya bahari na kukikaribia chombo; wakaogopa.
20-Naye akawaambia, Ni mimi, msiogope.
21-Basi wakataka kumpokea chomboni; na mara hiyo chombo kikaifikilia nchi waliyokuwa wakiiendea.

-Kwa nini wanafunzi waliogopa?

-Kwa sababu walimwona Yesu akitembea juu ya maji kuwaelekea.

-Mtu yeyote anaweza kutembea juu ya maji?

-La.

-Yesu tu ndiye aliyeweza kutembea juu ya maji.
-Hakuna mwingine aliye kama Yesu.

-Kwa sababu Yesu aliumba bahari, aliweza kutembea juu ya bahari.

-Kwa sababu Yesu ni Mungu, anaweza kufanya chochote anachochagua.

-Baadaye, umati wa watu ulienda kumtafuta Yesu.

Tusome Yohana 6:22-25

22-Siku ya pili yake mkutano waliosimama ng'ambo ya bahari waliona ya kuwa hakuna mashua nyingine huko ila moja, tena ya kuwa Yesu hakuingia katika mashua ile pamoja na wanafunzi wake, bali wanafunzi wake walikwenda peke yao.
23-(Walakini zikaja mashua nyingine kutoka Tiberia mpaka karibu na mahali pale walipokula mikate, wakati Bwana aliposhukuru.)
24-Basi, hao watu walipogundua kwamba Yesu na wanafunzi wake hawakuwapo mahali hapo, walipanda mashua, wakaenda Kaparnaumu wakimtafuta.
25-Wale watu walipomkuta Yesu ng'ambo ya pili wa ziwa walimwuliza, “Mwalimu, ulifika lini hapa?”

-Kwa nini umati ulikuwa ukimtafuta Yesu?



-Kwa sababu walimtaka awape chakula zaidi.

-Je, Yesu alijua kwa nini walikuwa wakimfuata?
-Ndiyo.

-Yesu alisema nini kwa umati?

Tusome Yohana 6:26-27

26-Yesu akawajibu, akasema, Amin, amin, nawaambieni, Ninyi mnanitafuta, si kwa sababu mliona ishara, bali kwa sababu mlikula ile mikate mkashiba.
27-Msikitendee kazi chakula chenye kuharibika, bali chakula kidumucho hata uzima wa milele; ambacho Mwana wa Adamu atawapa, kwa sababu huyo ndiye aliyetiwa muhuri na Baba, yaani, Mungu.

-Yesu aliwaambia umati kwamba walikuwa wakimtafuta tu kwa sababu alikuwa amewapa chakula.

-Kisha, Yesu akasema hivi:

-“Usifanyie kazi chakula kinachoharibika, bali chakula cha kudumu mpaka uzima wa milele.”

-Je, Yesu alimaanisha kuwa ni vibaya kufanya kazi ili kupata chakula chetu?
-La.
-Sote lazima tufanyie kazi chakula.

-Yesu alimaanisha nini?

-Yesu alikuwa anasema kuwa ni muhimu zaidi kufikiria juu ya chakula cha kiroho kuliko chakula cha mwili.

-Yesu alikuwa akisema kwamba ni muhimu kufanya kazi ili kupata chakula cha kiroho kuliko chakula cha mwili.

-Ni chakula gani cha kiroho ambacho tunapaswa kufanyia kazi?
-Neno la Mungu.

-Umati wa watu kisha ukamuuliza Yesu swali.

Tusome Yohana 6:28-29

28-Basi wakamwambia, Tufanyeje ili tupate kuzitenda kazi za Mungu?
29-Yesu akajibu, akawaambia, Hii ndiyo kazi ya Mungu, mmwamini yeye aliyetumwa na yeye.

-Watu walimwuliza nini Yesu?

-Walimwuliza Yesu ni kazi gani wanapaswa kufanya ili kumpendeza Mungu.

-Jibu la Yesu lilikuwa nini?

-Yesu alijibu kwamba kazi pekee inayompendeza Mungu ni kumwamini Yesu.



-Je watu walikubali yale Yesu alisema?
-La.

Tusome Yohana 6:30-31

30-Wakamwambia, Unafanya ishara gani basi, ili tuione tukakuamini? Unatenda kazi gani?
31-Baba zetu waliila mana jangwani kama vile ilivyoandikwa, Aliwapa chakula cha mbinguni ili wale.

-Watu walikuwa wakisema kwamba kama vile Musa alivyowapa Waisraeli mana kila siku jangwani, walitaka Yesu awape mkate kila siku.

-Yesu aliwajibu nini?

Tusome Yohana 6:32-33

32-Yesu akawaambia, Amin, amin, nawaambieni, Siye Musa aliyewapa chakula kile cha mbinguni, bali Baba yangu anawapa ninyi chakula cha kweli kitokacho mbinguni.
33-Kwa maana chakula cha Mungu ni kile kishukacho kutoka mbinguni na kuupa ulimwengu uzima.

-Je, Musa aliwapa Waisraeli mkate jangwani?
-La.

-Ni nani aliyewapa Waisraeli mkate jangwani?
-Mungu.

-Yesu alisema kwamba Mungu Baba ndiye aliyewapa Waisraeli mkate jangwani.

-Yesu alisema pia kwamba kama vile Mungu Baba alivyowapa Waisraeli mkate kutoka mbinguni jangwani, ndivyo Mungu Baba alikuwa akiwapa mkate wa kweli kutoka mbinguni.

-Mkate wa kweli kutoka mbinguni ambao Mungu Baba anatoa ni nani?
-Yesu.

-Je, Yesu anafananaje na mana ambayo Mungu aliwapa Waisraeli jangwani?

-Kama vile mana ilivyotoka mbinguni, ndivyo Yesu pia alikuja kutoka Mbinguni.

-Kama vile mana ilipewa na Mungu tu, ndivyo Yesu pia alipewa na Mungu tu.

-Kama vile Waisraeli wangekufa bila mana, ndivyo watu pia watakufa bila Yesu.

-Je watu walielewa?

Tusome Yohana 6:34

34-Basi wakamwambia, Bwana, sikuzote utupe chakula hiki.



-Watu hawakuelewa.

-Watu walidhani kwamba Yesu alikuwa anazungumza juu ya mkate kwa miili yao.

-Je, Yesu alikuwa anazungumza juu ya mkate kwa miili yao?
-La.

-Yesu alikuwa anazungumza juu ya mkate kwa roho yao.

Tusome Yohana 6:35

35-Yesu akawaambia, Mimi ndimi chakula cha uzima; yeye ajaye kwangu hataona njaa kabisa, naye aniaminiye hataona kiu kamwe.

-Yesu alisema kuwa alikuwa mkate wa kiroho kutoka mbinguni.

-Ikiwa mtu hatakula, je, atakufa?
-Ndiyo.

-Kama vile watu watakufa ikiwa hawali, ikiwa hatumwamini Yesu kama mkate pekee wa roho yetu, basi tutakufa pia.

-Kama tunamwamini Yesu, roho yetu haitakuwa na njaa tena.